# JARIBIO LA MTIHANI
## DARASA LA SITA – 001
## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

**Soma vifungu vifuatavyo. Kina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi, umepewa maneno manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa**

Mtoto ___1___ aliacha mchezo ___2___ aliokuwa nao na akafuata maneno ___3___ akiambiwa afuate na baba yake. Alitokea ___4___ mtoto ___5___ ___6___ wote ___7___ darasani ___8___, kwa hivyo mtihani ___9___ yeye ndiye ___10___ wa kwanza.

1. A. ule B. yule C. wale D. vile
2. A. yake B. zake C. wake D. lake
3. A. aliyokuwa B. aliokuwa C. alizokuwa D. alilokuwa
4. A. kua B. kuka C. kuwa D. kukuwa
5. A. mhodari B. hodari C. mbora D. mshujaa
6. A. kumliko B. kuwaliko C. kuliko D. kukiliko
7. A. huo B. hilo C. hiyo D. humo

9. A. mwao B. lao C. yao D. nao

9. A. ulikuja B. ulipokuja C. uliyekuja D. ilipokuja

10. A. atakayekuwa B. aliyekuwa C. angekuwa D. angalikuwa

Ama kweli, elimu ni bahari ___11___ haina mwisho. Kila siku, mja ___12___ jambo ___13___ ambalo hakulijua. Nayo elimu humfaa mmiliko wake kwa ___14___ na marefu. Mtu aliyesoma, kwa mfano, hupata kazi nzuri na hujua ___15___ na watu.

11. A. ambalo B. ambao C. ambaye D. ambayo
12. A. amejifunza B. anajifunza C. hujifunza D. atajifunza
13. A. mpya B. jipya C. mapya D. lipya
14. A. mapana B. mengi C. machache D. mageni
15. A. kutengana B. kutengemana C. kutangamana D. kutegana



PRINTED BY KISTE PRINTERS

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi**

16. Kitenzi 'choka' katika kauli ya kutendesha ni
    A. chokesha B. choza
    C. chosha D. chokea
17. Tumia kiunganishi mufti kujaza pengo
    Niliweza kumwua ndovu _______ swara
    A. laiti B. ilhali
    C. sembuse D. lakini
18. Udogo wa neno 'mwana' ni
    A. jijana B. jana
    C. kimwana D. kijana
19. Chagua kinyume cha neno lililopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo
    Baada ya <u>kutabasamu</u>, alianza kuhutubia hadhira
    A. kucheka B.kununa
    C. kughafilika D. kulia
20. Kamilisha methali ifuatayo
    A. Dua la kuku halimpati
    A. mjinga B. ndege
    C. mbwa D. mwewe
21. Sehemu ya chini ya sikio huitwa
    A. ndewe B. masharubu
    C. paji D. mashavu
22. Andika wingi wa sentensi ifuatayo.
    Mti uzaao embe unaitwa mwembe.
    A. Miti zizaazo miembe zinaitwa maembe.
    B. Miti izaay0 miembe inaitwa maembe.
    C. Miti izaayo maembe huitwa myembe.
    D. Miti izaayo maembe inaitwa miembe.
23. Jaza pengo kwa kivumishi kifaacho:
    Mtoto _______ alianguka vibaya sana.
    A. mwenye B. wenyewe
    C. mwenyewe D. enyewe
24. Mtu anayefanya kazi ya kujenga kwa mawe huitwa
    A. sonara B. mwashi
    C. hamali D. nokoa
25. Tegua kitendawili hiki
    Njoo umwone umpendaye.
    A. Kioo B. Picha
    C. Runinga D. Filamu
26. Malipo ya kuolewa huitwa
    A. nauli B. koto
    C. mahali D. mahari
27. Kanchiri, shimizi, kaptura na kocho kwa jina moja ni
    A. nguo B. mavazi
    C. mapambo D. maumbo
28. Bainisha akisami inayoonyesha subui
    A. $^{1}/_{7}$ B. $^{1}/_{3}$ C. $^{1}/_{8}$ D. $^{1}/_{8}$
29. Tumia '-ingine' kwa usahihi:
    Mama amenunua nguo _______ nyingi
    A. zingine B. ingine
    C. nyingine D. mengine
30. Tumia 'amba' kwa usahihi
    Mwalimu aliyeingia na vitabu ni Bwana Mirobi.
    A. Mwalimu ambaye anayeingia na vitabu ni Bwana Mirobi
    B. Mwalimu ambaye aliyeingia na vitabu ni Bwana Mirobi
    C. Mwalimu ambaye aingiaye na vitabu ni Bwana Mirobi
    D. Mwalimu ambaye aliingia na vitabu ni Bwana Mirobi.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40</u>***

Adili alijiandaa kwa safari ya kuitikia wito wa mfalme.

Farasi watatu walitandikwa matandiko mazuri. Yeye alipanda farasi mmoja, na mmoja kwa kila nyani. Ikibali alipanda farasi wake mwenyewe. Farasi wa Adili na yule wa Ikibali walikwenda sambamba njiani. Nyuma yao waliandamana nyani juu ya farasi. Kila mtu aliyeona nyani wamepanda farasi alistaajabu. Mnyama kupandwa na mnyama! Ulikuwa mpeo wa miujiza kwa watu.

Vinywa vya umati wa watu vilikuwa wazi kwa kivumo cha lo salala! Wakati umefika wa mawe kusema, miti kujibu na wanyama kuwa watu! Ikibali aligeuza uso wake kwa Adili akasema kwa ucheshi, "Mbwa wanatubwekea kama walionusa kundi la wanyama wanaowindwa." Adili alikubali kwa kuinamisha kichwa akitabasamu. Walisafiri hivi mpaka nchiya mfalme. Baada ya kutua, Adili alipelekwa mbele ya mfalme na manyani wake.

31. Adili alijizatiti kwenda
A. mkusaidia mfalme
B. kuonana na mfalme
C. kumwua mfalme
D. kuwatandika farasi

32. Farasi watatu waliotandikwa matandiko walikuwa ni wa kuwabeba
A. Mfalme, Adili na Ikibali
B. Adili, Ikibali na mfalme
C. Ikibali, Adili na nduguze
D. Adili na nyani wawili

33. Farasi wa Ikibali na wa Adili walikwenda sambamba. Maana yake ni kuwa walikwenda
A. mmoja mblele mwingine nyuma
B. karibu karibu
C. unyounyo mwendo wa asteaste
D. sawasawa ubavu kwa ubavu

34. Manyani waliandamana nyuma ya Ikibali na Adili. Ndiko kusema Adili na Ikibali waliandamana na nyani
A. sambamba
B. unyounyo
C. mkabala
D. chapuchapu

35. Kilichowashangaza watu zaidi katika habari hii ni
A. Adili kuongozana na Ikibali
B. Adili kupanda farasi
C. Nyani kupanda farasi
D. Mawe kusema, miti kujibu na wanyama kuwa watu

36. Ikibali aliposema kwa ucheshi, bila shaka
A. alinuna
B. alighadhabika
C. alinong'ona
D. alitabasamu

37. Mbwa alibweka. Je, wangekuwa fahali wangefanyaje?
A. Wengeroroma
B. Wangenguruma
C. Wangekoroma
D. Wangetetea

38. Ikibali alipogeuza uso wake kwa Adili, bila shaka
A. alimtazama Adili
B. alimpa Adili kisogo
C. alimkabidhi Adili
D. hakumwangalia ana kwa ana

39. Walipofika na kuwasili ughaibuni
A. mfalme waliwalaki
B. nyani walichoka
C. Adili na Ikibali waliagana
D. Adili alifikishwa maskanini pa mfalme

40. Kauli ipi si sahihi kulingana na makara haya?
A. Watu walishangazwa na nyani waliopanda farasi
B Watu walishangilia ili nyani wapande farasi
C. Mbwa nao waliobweka walipowaona Ikibali na Adili
D. Adili na nyani waliitwa na mfalme

***<u>Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 41 hadi 50</u>***

Zera Ahmed.
S.L.P 27001,
MOMBASA.
27-01-2001

Meneja Wa Benki Kuu,
S.L.P 20101,
NAIROBI.

KUH: OMBI LA KAZI

Mimi nina umri wa miaka thelathini, nimesomea kazi hii ya kufanya kazi kwenye benki kama mhasibu. Niliupata waraka mliokuwa mmetuma mkitafuta mhasibu. Mimi ni

mmoja wa wahasibu wale bora na maarufu zaidi nchini.

Nimeisomea kazi hii katika mojawapo wa vyuo vikuu nchini. Nilikuwa katika chuo kikuu kisha nikajaribu kufanya kazi kwa miaka miwili kwani nilikuwa nikijua kuwa, haba na haba hujaza kibaba.

Mimi ni stadi katika hisabati na lugha nyingine nyingi kama vile Kiswahili, King'eng'e, Kifaransa, Kijerumani pamoja na lugha nyingine nyingi.

Sipendi mapendeleo labda katika kabila, aila au hata rangi ya sura.

Huu ndio mwanya peke yake ninao wa kupata kazi hii ya uhasibu. Tafadhali ninakusihi unipe kazi hii.

Wako mwaminifu,

Zena Ahmed.

---

41. Barua ya aina hii huitwa
   A. barua ya kindugu
   B. barua ya kirafiki
   C. barua rasmi
   D. barua kuu
42. Anwani ya pili katika barua hii ni ya
   A. mwandishi
   B. mwandikiwa
   C. Zena
   D. mhasibu
43. Barua hii iliandikwa mwezi gani?
   A. Februari
   B. Machi
   C. Juni
   D. Januari
44. Nia ya mwandishi huyu kuandika barua hii ni
   A. kuwa meneja
   B. kuenda chuo kikuu
   C. kuwa tarishi wa benki
   D. ombi la kazi katika benki
45. Mwandishi amesomea kasi ya
   A. utabibu
   B. uhasibu
   C. ualimu
   D. ukadamu
46. Kazi ya uhasibu ni ipi?
   A. Kazi ya kuhesabu pesa
   B. Amali ya kuchunga pesa
   C. Riziki ya upelelezi
   D. Kazi ya ufundi
47. Baadhi ya mapendeleo ambayo mwandishi hayapendi na yametajwa ni kama vile
   A. ukabila
   B. jinsia
   C. lugha
   D. elimu
48. Mwandishi wa habari hii amesoma hadi
   A. shule ya msingi
   B. chuo kikuu
   C. shule ya upili
   D. chekechea
49. Zena Ahmed alisomea kazi hii ya uhasibu wapi?
   A. Chuo kikuu
   B. Shule ya upili
   C. Shule ya msingi
   D. Chuo cha ufundi
50. Mwandishi wa habari aliandika barua akiwa wapi?
   A. Makerere
   B. Mombasa
   C. Benki
   D. Nairobi